# MAHUSIANO 102

## KUITAMBUA DHAHABU KATIKATI YA MCHANGA

JAMES KALEKWA

# MAHUSIANO 102:

*Kuitambua dhahabu katikati ya mchanga.*

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

1. Kujitambua ........................................................ 4

*a) Thamani inayoanzia ndani kuja nje* ........................... 4

*b) Mimi ni nani na mimi siyo nani* ................................. 8

2. Kufanya kazi kwa bidii ............................................ 9

3. Kujidhabihu ........................................................ 12

4. Utii na Unyenyekevu ............................................. 13

5. Ujasiri kusimamia mambo ya msingi ............................ 14

Mawazo ya Mchungaji: ................................................ 14

Funzo: .................................................................. 16

Soko la Ndoa: Ni wapi pa kumpata mwenzi? ........................ 17

Kisa cha "Bucha" za kisasa: ......................................... 18

Upande wa pili wa sarafu: ............................................ 19

Mtego unaonasa wengi ................................................. 20

# 1. Kujitambua

*a) Thamani inayoanzia ndani kuja nje*

*"Mimi ni mweusi-mweusi [kwa nje], lakini ninao uzuri [wa ndani]..."* Wimbo Uliobora 1:5a [mkazo uliowekwa kwenye mabano ni wa mwandishi].

Inawezekana katiba kwenye zama za vijana hawa kulikuwa kuna vipimio vinavyokubalika vya uzuri. Kwa maandishi haya inaonyesha ya kwamba vipimo vilikuwa ni vigezo vya rangi. Walau kutokea kwenye midomo ya binti kuwalekea "wapinzani" wake ni kwamba kipimo cha uzuri hakikuwa rangi nyeusi, ambayo binti huyu alikuwa nayo.

Hata hivyo, hiyo haikumsababisha ajiseme kuwa ni mbaya (si mzuri), bado alikaza ya kwamba yeye ni mzuri.

Kwenye mazingira yetu, tumepewa tafsiri za uzuri kutoka kwenye mashidano ya ulimbwende, mitandao ya kijamii, na watu maarufu (celebrities). Ambao kimsingi uwekezaji mwingi wa uzuri huu hufanyika nje tu na ukichunguza kwa umakini utagundua nyuma ya huo uzuri kuna uvundo!

Maandiko matakatifu husema hivi kuhusu uzuri na kujipamba:

*“3. Kujipambana kwenu kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi.”*
*“4. Bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani roho ya upole na utulivu. Iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu.”*
*“5. Maana hivyo ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu, na kuwatii waume zao.”*
**1 Petro 3:3-5**

Unaona mkazo wa kujipamba? Ni kutokea ndani kwenda nje; au kwa lugha nyingine, hapa ni mkazo wa vipaumbele. Mambo ya kwanza acha yafanyike kwanza (first things first). Unaupamba utu usioonekana ambao kimsingi huyo ndiye wewe halisi. Ukifanya hivyo utakuwa unajipamba wewe! Mzee Petro anatupa kina zaidi kubainisha ya kwamba yanayotumika kukupamba wewe halisi ni *“mapambo yasiyoharibika”*. Kinyume chake, mapambo ya nje huharibika – yaani huwa na expiry dates, hufifia, hupitwa na wakati, huisha… na hata hivyo, mtu huyavua na kuyavaa (si ya muda wote).

Mapambo yenyewe sasa yanayotajwa; roho ya **upole** na **utulivu**; kumbe mapambo yenyewe ni “roho” na si

vipodozi! Utagundua ya kwamba hakuna duka linauza mapambo haya; utagundua hata wasio na fedha ya kununua vipodozi, wanaweza "kununua" roho ya upole na utulivu.

Ulishawahi kusikia mashindano ya ulimbwende ambapo kigezo kimojawapo cha kunyakua taji ni roho ya upole na utulivu? La hasha! Inawezekana hata waamuzi hawana mapambo hayo wao wenyewe.

Si ajabu binti ilibidi ajisemee mwenyewe *"…lakini ninao uzuri…"* kwa sababu kwa vipimo vya uzuri vya wakati wake, huenda "waamuzi" wasingeona huo uzuri;

Nimewahi kuandika ushairi kuchokoza ufikiri kwenye eneo hili. Hebu fikiri pamoja nami:

> **Urembo ni Uzuri?**
> Na Pastor JK
> Jamaa watafutao hutafuta mzuri,
> Mzuri kwao wapimiacho sijui

Kwa hili, kichwani mi sifuri
Ndiyo maana nauliza, urembo ni uzuri?

Acha nianike wangu usifuri
Ili nisaidike kwa kuchorea mstari
Kuna wale wajipambao manukato na uturi
Na hao ndo huonekana ng'aring'ari
Ndiyo maana nauliza, urembo ni uzuri?

Wale wajipakao wanja na rangi-rangi
Husema ni mwonekano uvutiao wengi
Hilo haliondoi swali langu la msingi
Ndani au nje: upi mwonekano wa msingi?
Ndiyo maana nauliza urembo ni uzuri?

Kuna wale wajikwatuao kwatukwatu
Kwa pambo la nywele mpaka kiatu
Na huo hasa ndo mwonekano uvutiao watu
Hapa gharama ni fedha pamoja na vitu
Ndiyo maana nauliza, urembo ni uzuri?

Niliwahi kudokezwa na wajuao kw aundani
Eti uzuri unazaliwa nao urembo ni wa dukani
Uzuri jambo la ndani, urembo ni hadharani
Urembo ajili ya picha, uzuri ni maishani
Ndiyo maana nauliza, urembo ni uzuri?

Mjuzi alin’dokeza urembo unashikika
Kaongeza kusema uzuri huheshimika
Nami nikahoji “Vitu hivi vyapimika?”
Lau nijue kipi hubaki mtu anapozeeka
Ndiyo maana nauliza, urembo ni uzuri?

Marefu yaso nan cha hakuna
Naacha nafasi ya wengine kunena
Majawabu yalochimbwa toka kina
Nataraji kusikia akijalia Rabana
Mtunzania kujibiwa kama urembo ni uzuri.

*b) Mimi ni nani na mimi siyo nani*

Kujitambua ni kuchora mpaka; kujitambua ni kujitofautisha. Ukweli usiopinguika ni kwamba wewe si kila kitu. Tena ni vizuri ikuingie akili ya kwamba wewe huna “sifa” zote za kuwakidhi wanadamu wote duniani. Hii ni moja ya maajabu ya Mungu aliyoyaumba duniani. Ni vyema kujua wewe ni nani, umekirimiwa nini, umebarikiwa nini, una uwezo na uwezsho gani… na wewe si nani na huna nini; na kama vile unavyokubali uliyokirimiwa nayo, ukubali pia usiyokuwa nayo

> ***“Mimi ni mweusi-mweusi [kwa nje], lakini ninao uzuri [wa ndani]…”*** Wimbo Uliobora

1:5a [mkazo uliowekwa kwenye mabano ni wa mwandishi].

Hii itakupunguzia presha ya “mbwa kukimbiza mkiwa wake”.

Kujitambua kwa namna hii hukusaidia kutambua *mambo ambayo huwezi kuyabadilisha*. Kwa mfano, binti huyu anaelezea kigezo cha uzuri ambacho ni rangi ya ngozi. Asingeweza kukibadili ili awe “mzuri” sawasawa na mabinti wenzake anaowaita “binti za Yerusalemu”. Kwneye mambo ya namna hii, mwitikio wako unapaswa kuyapokea na kuyakubali.

Upande mwingine, itakusaidia kutambua mambo ambayo kwa wakati huo huna lakini unaweza kuyatafauta na kuyapata.

Mtu asiyejitambua kwa umbali huu huishi kwa kujidanganya nafsi yake yeye mwenyewe.

## 2. Kufanya kazi kwa bidii

“Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi-mweusi, Kwa sababu jua limeniunguza. Wana wa mamangu walinikasirikia, Waliniweka niwe **mlinzi wa mashamba ya mizabibu**; Bali shamba langu mwenyewe sikulilinda.”

Wimbo Uliobora 1:6

Kwenye muktadha wa andiko hili, binti mshulani anaanza kuutambulisha uzuri wake wa ndani – uzuri wa kitabia. Anaeleza ya kwamba aliwekwa kuwa *“…mlinzi wa mashamba ya mizabibu…”.*

Kwanza, tambua ya kwamba mwanamke kiutamaduni hakuwa mlinzi na hakuwa mtu wa kutenda kazi mashambani (field). Hata hivyo, huyu mwanamke ni “jembe”. Ni wana (sons) wa mama yake, kaka zake wa kufikia, ndiyo waliomshurutisha kufanya kazi ya ulinzi. Huenda lilikuwa ni jukumu lao kimsingi, wakalihalimishia kwake.

Pili, ninataka uone uzito wa kazi. Unafikiri mlinzi wa mashamba ya mizabibu hulinda dhidi ya akina nani? Yaani, ni wanyama gani huja kushambulia mashamba ya mizabibu?,.. ndiyo, kwanza ni wanadamu. Kuna wanyama kama mbweha ambao huvamia mashamba. Hii ndiyo kazi aliyofanya huyu binti. Mlinzi hufanya kazi kwenye hali zote – jua na mvua; upepo na dhoruba; ni kazi ya muda wote.

Tatu, umegundua kwamba alifanya kazi kiasi kwamba kazi ilimuachia alama kwenye mwili wake? *“Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi-mweusi, Kwa sababu jua limeniunguza…”* anatuonyesha kwamba kimsingi yeye si mweusi bali ni mweusi-mweusi. Ndiyo kusema hilo rangi ya ngozi ni matokeo ya kukaa

juani muda mrefu akifanya kazi yake ya ulinzi kwa uaminifu. Hiyo ndiyo alama yake ya bidii ya kazi.

Niambie ni mwanamume gani asingependa kuoa mwanamke mwenye bidii namna hii?

Upande wa pili, kijana naye hakuwa haba. Alikuwa ni mtu wa bidii kwenye kazi zake pia.

“Nijulishe, ee mpendwa wa nafsi yangu, ***Ni wapi utakapolisha kundi lako, Ni wapi utakapolilaza adhuhuri***. Kwa nini niwe kama aliyefungiwa kidoto, Karibu na makundi ya wenzako?”

Wimbo Uliobora 1:7

Ni kijana aliyekuwa kwenye kazi ya kulisha makundi yake ya wanyama wa kufuga. Alihakikisha makundi yake anayalisha na kuyalaza wakati wa adhuhuri. Unakumbuka kuhusu Zaburi 23? Unaona kazi ya uchungaji aliyokuwa nayo huyu kijana?

Dada, kama kuna kijana anaonesha kuvutiwa na wewe, hakikisha unampimia kwenye bidii yake kazi. Na kama kuna mtu wa bidii anakusogelea, hiyo ni sifa ya dhahabu.

## 3. Kujidhabihu

“Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi-mweusi, Kwa sababu jua limeniunguza. Wana wa mamangu walinikasirikia, Waliniweka niwe mlinzi wa mashamba ya mizabibu; **Bali shamba langu mwenyewe sikulilinda.**”

Hii ni tabia ya kwenda hatua kubwa zaidi ya unavyotarajiwa au ulivyopangiwa. Ni kuchagua kuahirisha mambo yako ili wengine wapate manufaa. Wakati ninaandika kitabu hiki nina miaka 7+ kwenye ndoa; ni kweli sijaona mambo yote, hata hivyo nimeona kiasi cha kufikia hitimisho ya kwamba kwenye ndoa kuna majukumu! Na mara nyingi yatakutaka kuwawazia watu wa nyumbani mwako kabla hata yako wewe mwenyewe… utajikuta unalinda mashamba ya mizabibu ya watu wako, na shamba lako hutalilinda.

Kwa andiko hili tunaona namna gani huyu binti aliamua kudhabihu shamba lake mwenyewe na kuamua kuwekeza muda kulinda mashamba ya wana wa mama yake. Wengine hutafsiri ya kwamba, shamba lake ni mwili wake ambao uligeuka na kuwa mweusi-mweusi. Hakuwekeza muda kuuvika mapambo kwa muda ili akamilishe kazi ya ulinzi.

Mtu ambaye yuko radhi kuchelewesha au kuahirisha ridhiko lake kwa muda kwa sababu ya wengine ni mtu wa kujidhabihu… na hiyo ni dhahabu!

## 4. Utii na Unyenyekevu

"Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi-mweusi, Kwa sababu jua limeniunguza. **Wana wa mamangu** walinikasirikia, Waliniweka niwe mlinzi wa mashamba ya mizabibu; Bali shamba langu mwenyewe sikulilinda."

Moja yapo ya siri anayotufunulia binti huyu ni mtu mtii na mnyenyekevu; amejiweka chini ya mamlaka na maelekezo ya wana wa mama yake (kaka zake wa kufikia). Walimpa maelekezo; walimuhamishia majukumu yao ya kimsingi… tena inaonekana walifanya uonevu au kwa chuki. Hata hivyo, bado binti alibakia kwenye hali ya utii.

Namna nzuri ya kuitambua dhahabu, angalia namna gani mtu huyo anahusiana na wazazi wake, ndugu zake na watu wenye mamlaka na amri juu yake. Mtu aliye na shida kukaa chini ya mamlaka na malekezo, hupata shida sana kutiririka kwenye utaratibu na mamlaka.

Je, huyu "mchumba" ni mtu wa mabishano, mizozo, mgumu kuomba msamaha, asiyetaka suluhu?

Hata kama ni mambo yaliyofanyika kwa uonevu, bado unaweza kufuata utaratibu wa namna ya kuyashughulikia.

## 5. Ujasiri kusimamia mambo ya msingi

"5. Mimi ni mweusi-mweusi, lakini ninao uzuri, Enyi binti za Yerusalemu. Mfano wa hema za Kedari, Kama mapazia ya Sulemani 6. Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi-mweusi, Kwa sababu jua limeniunguza. Wana wa mamangu walinikasirikia, Waliniweka niwe mlinzi wa mashamba ya mizabibu; Bali shamba langu mwenyewe sikulilinda." **Wimbo Uliobora 1:5-6**

Ukisoma andiko hilo utagundua kulikuwa na kundi kubwa [sijui ni kubwa kiasi gani] la mabinti ambao walikuwa na upendo kumulekea kijana wa kiume. *"… kwa hiyo wanawali hukupenda…"* Wimbo Uliobora 1:2b

Ndilo kundi ambalo binti mshulami anazungumza nalo tena wenye mstari 5-6. Anaongea nao na kuwaambia *"…msinichunguze…"*.

### Mawazo ya Mchungaji:

Kila nikisoma andiko hili huwa ninajenga taswira ya binti mwenye nguo zilizojaa vumbi, aliyepauka kwa vumbi, aliyechoka kwa jua la siku, mwenye ngozi

iliyofifia (isiyo na nuru), nywele kichwani zimevurugika… hana chembe ya mvuto. Ninamuona binti huyu anatokea mashambani hali akitembea kwa miguu; namuona akitembea watu wanamtazama na kumcheka kwa sababu ni binti kituko. Anapita mjini (kwa sababu mjini ni katikati ya shambani na nyumbani kwao – hawezi kupakwepa), anakutana na mabinti wenzake waliokuwa naye kwenye mafunzo (kufundwa) ya kuwa mwanamke – wanawali! Wameoga na kupaka mafuta na manukato; wamejikwatua kwa mapambo mbalimbali, wantembea hapa na pale ilimradi wanaume wa mjini wawaone. Wakimuona wanashindwa kujizuia, wanamsogelea, wanabetua nywele zake, wanashikashika ngozi yake kama vile wanamuondolea vumbi au tope lililogandamana… wanajiridhisha sauti ni yake, macho ni yake, ufahamu ni wake… LAKINI amechakaa sana. Amekuwa mweusi-mweusi. Wanaendelea kumchunguza.

Jambo hili linaendelea kufanyika mpaka pale anapowasili kijana ambaye wote wamekuwa wakivutiwa naye. Anapotokeza, kila mmoja anamtazama kama vile kumwambia *“nisemeshe basi!”.* Halafu pasipo kujibu lolote, yule kijana anawatazama kwa kuwakazia macho kama kutokukubaliana nao; kisha kwa hali ya tabasamu na unyenyekevu anamgeukia yule binti “mshamba” na kumshika

mkono na kumwambia *“Twende nikupeleke nyumbani kwenu, usiku unaingia.”*

Haya ni mawazo yangu tu ninaposoma Biblia. Huwa ninaona taswira.

Jambo hili linaendelea mara nyingi, kiasi kwamba Binti za Yerusalemu (wadada wa mjini) wanajipanga kumshambulia kwa maneno binti mwenzao. Siku hiyo, binti anapita mjini na bila salamu wala nini, wanaanza kumrushia maneno… baada ya kuwasikiliza, binti waliyedhani ni mnyonge, mlegevu na dhaifu anaamua kujibu mapigo. Ninamuona amesimama kwa ujasiri, amewakazia macho na kuwakabili wataabishaji wake, anawanyooshea kidole na kuwaambia:

“5. Mimi ni mweusi-mweusi, lakini ninao uzuri, Enyi binti za Yerusalemu. Mfano wa hema za Kedari, Kama mapazia ya Sulemani 6. Msinichunguze kwa kuwa ni mweusi-mweusi, Kwa sababu jua limeniunguza. Wana wa mamangu walinikasirikia, Waliniweka niwe mlinzi wa mashamba ya mizabibu; Bali shamba langu mwenyewe sikulilinda.” **Wimbo Uliobora 1:5-6**

## Funzo:

*“Watoto wa mjini”* wengi watataka kushambulia mambo ya kimsingi na maadili; watataka uonekane mshamba na uliyepitwa na wakati kwa kusimamia

mambo ya msingi. Unapaswa kukabili dhihaka hizo mpaka *"washike adabu yao."*

Siyo unatikiswa kidogo tu, unaicha njia. Siyo wokovu unasemwa vibaya, utakatifu na usafi unatukanwa, unadhihakiwa au unaonekana ni ushamba na wewe unanywea na kujikunyata. Kuwa jasiri kwenye mambo ya msingi na ya kikanuni.

*"... bali wenye haki ni wajasiri kama samba."* **Mithali 28:1**

## Soko la Ndoa: Ni wapi pa kumpata mwenzi?

*"Ukitaka kuchagua mwenzi usichague ngomani, chagua shambani"* – Methali ya Kiafrika

Kuna dhana imejengeka miongoni mwa vijana wengi ya kwamba umri fulani ukiwadia ni muda wao wa kuingia kwenye "soko la ndoa". Huingia kwa nafasi zote, kama bidhaa na kama wanunuzi. Dhana hii imeleta mchanganyo kwa wengi.

Ukienda kwa dhana hii, kama bidhaa ndani ya soko, mara nyingi utahakikisha umejifanyia *"packaging"* kulingana na uhitaji wa soko. Na hii imepelekea wengi kuwa radhi kufanya chochote kinachowezekana bidhaa isilale; na wengine wamefika mahala pa kupindisha kanuni na mambo ya kimsingi kama vile

imani, uchaji na utakatifu ili tu wanunulike kama bidhaa sokoni. Kwa kujua au kutokujua, unajikuta kijana umekuwa “msanii” – unaigiza maisha ili kuvutia wateja.

Kisa cha “Bucha” za kisasa:

Ninaamini unayafahamu maduka ya kuuza nyama za aina mbalimbali yajulikanayo kama bucha! Siku moja, mimi na mke wangu (na binti yetu Priscilla) tulitoka nyumbani na kuendesha gari kuzungukia maeneo fulani ya mji wa Dodoma. Mara kadhaa huwa tunafanya hivyo kama sehemu ya kuufahamu mji na kuusemesha kama watumishi wa Mungu. Tukafika kwenye eneo fulani ambalo kulikuwa na bucha kadhaa ambazo tulivutiwa kwa kuona mabango yao ya mlangoni. Mke wangu akapendelea kwenda kuchua kitoweo cha kuku. Kabla hajaenda alisema sentensi ambayo ilinipa kufikiri sana. Alisema, *“Hizi bucha za siku hizi wanabandika picha zinavutia sana kwenye milango. Na kumbe nyama inayouzwa si kama ile ya kwenye picha. Picha zilizohaririwa za mitandaoni, na nyama ni ya hapa uraiani.”*… tukacheka hali nikiwa kwenye hali ya kuyatafakari aliyoyasema, akaongeza tena, *“… hawa jamaa wangeweza kuhariri nyama wangefanya hivyo ili wapate wateja. Ila nyama huwezi kuihariri.”* Kisha akaniacha mimi na Priscilla ndani ya gari akaenda kununua nyama “isiyohaririwa”

Baada ya kurudi nilimshirikisha tafakari yangu juu ya "Utamaduni wa Soko" [the market culture] kutokea kwenye maneno yake na hatimaye tukaenda kujadili mpaka matokeo ya "Utamaduni wa Soko" kwenye maswala ya ndoa. Vifungashio [packages] na mbao za matangazo zimekuwa za kuvutia mno huenda kuliko hata bidhaa yenyewe.

## Upande wa pili wa sarafu:

Kwa upande mwingine, ukiwa kama mnunuaji wa bidhaa sokoni. Utamaduni huu wa soko umewafanya vijana wengi kuwa na matarajio hewa; matarajio yasiyo na uhalisia. Wengi hudhani mahusiano/ndoa ni bidhaa iliyokamilika na kufungwa kwenye vifungashio tayari kwenda kwa mlaji wa mwisho [final consumer], ambaye kwa akili hii ya utamaduni wa soko – mlaji huyo ni wewe!

Na kumbe baada ya kufungua vifungashio vizuri walivyowekewa kwa juu wanagundua wamenunua "nyama mbichi". Ni wajibu wao kuchoma, kukaanga, kuchemsha; au iwe mishikaki, iwe rosti… Yaani, wao ndiyo waamuzi wa pishi! Na kwa vile wengi hawajui "kupika mahusiano" ndipo huishikashika nyama na kuitupa.

Nilibahatika kufundishwa nikiwa kijana mdogo wa miaka kumi na kitu hivi ya kwamba raha ya mahusiano si ile bidhaa ya mwisho bali ule mchakato unaokupelekea kupata bidhaa.

Ulishawahi kusikia usemi wa "jasho la mtu haliliwi"? Basi, ukiona bidhaa yoyote imekamilika ujue kuna jasho la mtu. N akwenye ulimwengu wa mahusiano, uwe na uhakika "jasho la mtu haliliwi" kweli!

## Mtego unaonasa wengi

Ni nani angependa kuoa mwanamke mwenye jeraha la kazi? Ni nani angependa kuolewa na mwanamume ambaye kutwa anachunga makundi ya wanyama? Ni nani angependa mwenzi ambaye "shamba lake mwenyewe" hakulilinda?... HAKUNA!

Kwa bahati mbaya sana hizo ndizo sifa za dhahabu!

Kuna tofauti kubwa kati ya dhahabu ghafi (raw) na iliyosafiwa. Dhahabu ghafi huwa imefunikwa na mchanga. Kiasi kwamba mtu ambaye hajafundishwa kuyatambua madini, hawezi kuichukulia kwa uthamani wake. Huwa imefunikwa na mchanga na udongo mwingi. Hufanana na mawe mengine; huwa kama mabonge ya udongo; huwa kama miamba tu. Lakini hayo hayaubadilishinukweli ya kwamba hiyo ni dhahabu. Inahitaji kusafiwa tu!

Vijana wengi huzitazama ndoa za watu wanaowahusudu na kuishia kutamka *“mke kama wa fulani”* au kuoelewa na *“mume kama wa fulani”*. Laiti wangejua wanachokitazama ni dhahabu safi. Habari si ya kufurahisha kwa watu wa namna hiyo ni kwamba dhahabu zote safi zimenunuliwa na zinamilikiwa na wenyewe! Utaishia kutamani wake za watu na/au waume za watu – acha mara moja!

Dhahabu ghafi zina mwonekano usiovutia. Jifunze kukaza jicho ili kung’amua thamani zaidi ya thamani inayoonekana kwa juu-juu.

Ndiyo, ni mweusi-mweusi…

Ndiyo, ni mchungaji wa kundi la kondoo kutwa nzima…

Ndiyo, analinda kwenye shamba la mizabibu…

Lakini kama ana bidii, unyenyekevu, utii, anajitambua… hiyo ni dhahabu! Chukua haraka sana, ifiche, isafishe.

Hivi unafahamu hata ile rangi ya ngozi ya binti mshulami “mweusi-mweusi” [ambao kwa watu wa wakati wake walimtazama kama mwanamke asiye na mvuto] haikuwa rangi yake ya asili bali ni alama ya kazi yake ya ulinzi wa mashamba ya mizabibu? Hiyo ni kusema ya kwamba, binti huyo akipata mume wa kumtunza nyumbani, asiwe kwenye mashamba ya

mizabibu ili "shamba lake mwenyewe alilinde" atakuwa ni binti mrembo wa kuvutia.

Neno la Kristo linasema hivi:

*"Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; 26. Ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno 27. Apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa."*

Waefeso 5:25-27

Utagundua ya kwamba Kristo alilifuata kanisa likiwa "kwenye mchanga" akalisafisha na kulitakasa kiasi kwamba likawa ni jumuiya yenye nguvu sana kuwahikutokea ulimwenguni.

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: [https://www.newvinechurch.or.tz](https://www.newvinechurch.or.tz)

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi n audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: [https://t.me/nvcdodoma](https://t.me/nvcdodoma) AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa

james_kalekwa

@MchungajiJK

+255 754 917 764